# JE WAWEZA KUA MKRISTO KWA JINA TU ILA HUJABADILIKA?

Unaweza kujua kwa njia gani kwamba wewe ni Mkristo? Je, kunayo kiwango fulani mtu anahitajika kufikia ndipo aweze kuitwa Mkristo kwa uhalisi? Biblia inatoa ilani dhidi mafundisho ya uongo itakapotosha wengi. Mtu anaweza kutambua mafundisho ya uongo kwa njia gani ili kutopotoshwa?

Tuchukue kwa mfano mtu ambaye anamkubali Yesu kama Bwana na Mkombozi, ambaye kwa imani huenda kanisani kila Jumamosi au Jumapili, ambaye hajawahi kamwe kuzini, na huonyesha upendo kwa kila mmoja? Utamtambua mtu huyo kama Mkristo?

**Kumwabudu Kristo Hautoshi**

Wengi watamchukua mtu huyu kama Mkristo kwa sababu anamkubali na kumwabudu Yesu Kristo kama Bwana na Mkombozi. Walakini, habari ya kustaajabisha kutoka kwa Biblia ni kwamba kukubali na kuelekeza maombi yako kwake Yesu haikufanyi kuwa Mkristo! Yesu anaiweka hii wazi katika Marko 7:7-8: *"Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.* Ninyi mwaiacha amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu."

Kristo hawezi kubali ibada zetu ikiwa hazikubaliani na amri za Mungu. Ikiwa ibada zetu haziwezi kubaliana na amri za Mungu, basi ni za kubuniwa *kibinadamu!* Tamaduni za kubuniwa kibinadamu ni mazoezi za ibada ambazo hazijaagizwa na Mungu. Kwa mfano, sherehe za krismasi, pasaka, na Jumapili kama siku ya Kikristo ya ibada hazina asili kutoka kwa Biblia. Mazoezi hizi za ibada ni tamaduni za kubuniwa kibinadamu na hazikubaliki kwa Mungu. Ibada inakubaliwa na Mungu ikiwa inakubaliana na amri zake. Kwa hivyo, Yesu anatoa ilani, "Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 7:21).

Wengi huamini kwamba hakuna kazi za kulekeza kwa wokovu, na kwamba mmoja anapaswa tu kumwamini Bwana Yesu ili aweze kupata wokovu. Lakini Yesu anatupilia mbali maoni hiyo anapouliza, "Na kwa nini mnaniita, Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?" (Luka 6:46). Mashetani nao waamini na kutetemeka (Yakobo 2:19), lakini hio haiwafanyi kuwa Wakristo.

Kwa hivyo ni muhimu kwa kila mmoja amtafutaye Mungu kujua kile kilicho ukristo wa kweli na ule wa uongo. Mtume Yohana anatuhimiza, "Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu" (1 Yohana 4:1). Tunawezaje kujaribu hizi roho? Wengine wanaamini kwamba Roho ya Mungu ni wazi kwa kufanya miujiza. Wengine hutazama mafanikio ya makutano ya kievanjelisti kama dhihirisho kwamba Mungu anawatumia, wakati

wengine wanatazama hekima, shughuli, na uwazi wa mhubiri. Lakini je, hizi ndizo nguzo za kushikamana nazo kwa kujaribu roho hizi?

**Miujiza Haitoshi**

Bila shaka, tunamtumikia Mungu mwenye kazi za miujiza, lakini Biblia pia huiweka wazi kwamba ishara na ajabu sio dhihirisho ya Roho ya Mungu kazini. Mitume Paulo na Yohana wanazungumzia miujiza za *uongo* katika siku za mwisho zikifanywa na wanadamu waasi (wale wasiozitazama sheria za Mungu).

"Yule ambaye kuja kwake ni kwa mfano wa kutenda kwake *shetani*, kwa uwezo wote na ishara na ajabu za uongo; na katika madanganyo yote ya udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli, wapate kuokolewa" (2 Wathesalonike 2:9-10).

"Naye [yule mwasi] afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi" (Ufunuo 13:13-14).

Tazama hiyo miujiza ya nguvu ikitumika katika siku za mwisho itawapotosha wanadamu wengi. Haya ni miujiza ambazo hufanyika; watu kwa kweli huponywa. Lakini Biblia huzitambua kama za uongo kwa sababu Roho ya Mungu hazifanyi, vile miujiza ya Farao ya kugeuza fimbo lake kuwa nyoka haikufanywa na Roho ya Mungu. Hii ndio sababu Mungu anatutarajia kujaribu roho hizo. Ulimwengu wa kiroho ni wa nguvu, na kama wanadamu tunaweza kuchukuliwa na kazi za roho za uovu, na kuziamini kama kazi za Mungu.

Hebu fikiria, kwa mfano, mama akiwa mlemavu kwa miaka ishirini na makutano ya uponyaji unakuja katika eneo lako. Upendo wako kwa mama yako na matamanio yako kumwona akiponywa inakutia motisha kumpeleka kwa uponyaji. Ni furaha gani utakapomwona akiamka kutoka kitini mwake akiruka kwa furaha na kumshukuru Yesu. Mtu yeyote anawezaje kukushawishi kwamba hii haikuwa kazi ya Roho Mtakatifu, kwa kuwa umekuwa ukiomba juu ya hali ya mama yako kupitia miaka mingi? Mbona ungetaka kumsikiliza yeyote anayekuambia kwamba hii haikuwa kazi ya Yesu Kristo wakati wewe binafsi uliona miujiza hiyo ya nguvu mwenyewe? Hii ndio hasa kile Yesu alituonya alipowaambia wanafunzi wake kwamba "makristo wa uongo na manabii wa uongo watatoa ishara na maajabu, wapate kuwadanganya, kama yamkini, hata hao wateule" (Marko 13:22).

Watu wanadanganywa kwa sababu wanachukuliwa na hisia zao na kukataa kuchunguza ukweli wa Biblia dhidi ya imani na mazoezi ya wale wanaodai kumwakilisha Kristo. Kwa hivyo badala ya kuonyesha nguvu ya Roho wa Mungu, mengi ya kazi ya miujiza katika siku za mwisho zinahusiana na kazi za shetani.

**Kuwa na Waumini Wengi Hautoshi**

Wengi hutazama runinga zao na kustajabishwa na umati wa watu wanaokwenda kwenye madhehebu wakilia ili wampe Kristo maisha yao. Waevanjalisti wa runinga wanatoa hii kama dhibitisho wa mkono wa Mungu wa nguvu kazini na pia sababu mzuri kwa watazamaji wao ili kusaidia kazi zao. Yeyote hapaswi kuuliza maadili ya evanjelisti huyo lakini ni muhimu kuchunguza ikiwa waumini wengi ni dhihirisho ya kazi ya Roho wa Mungu.

Biblia hutambua waumini wengi kama wale wanaopotoshwa, sio wale wanaoupata ukweli. Yesu anaelezea kanisa lake kama "kundi dogo." "Msiogope, enyi kundi dogo; kwa kuwa Baba ynu ameona vema kuwapa ule ufalme" (Luka 12:32). Mmoja anaweza kutoa hoja kwamba kanisa lilikuwa kundi dogo wakati ulipoanzilishwa na Yesu lakini lilipaswa kuwa kundi kikubwa. Yesu, hata hivyo, anasema juu ya *kuendelea* kwa kundi hili dogo anaposema, "Bali mlango ni mwemamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache" (Mathayo 7:14). Kwa hivyo watu wa Mungu hawatambuliwi kwa makanisa makubwa walio na waumini wengi. Lakini mtu hapaswi kuchukua hii kumanisha hivyo kwa sababu kundi dogo ni ya Mungu. Hoja hapa ni kwamba mmoja hapaswi kudanganywa na umati mkubwa kwa kuamini kwamba hii ni kazi ya Mungu. Kwa kweli, Biblia huhusisha kazi za shetani na umati mkubwa kuelekea nyakati za mwisho. "Naye [yule mnyama] afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu. Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama…" (Ufunuo 13:13-14).

Biblia hufundisha kwamba wengi watakuja kujua ukweli tu na kumjua Yesu Kristo wakati wa Milenia baada ya kurudi kwa Kristo. Wakati huo, Shetani atafungiwa asiweze kuwadanganya mataifa tena na kisha kufunguliwa mda mchache mwishoni mwa milenia (Ufunuo 20:1-5).

**Mtu Anawezaje Kutofautisha Ukristo wa Kweli na wa Uongo?**

Mtu anawezaje kutofautisha ukristo wa kweli na wa uongo? Tunajuaje watumishi wa kweli wa Mungu? Yesu anatuambia. Katika Luka 6:46, anasema, "Na kwa nini mnaniita, 'Bwana, Bwana,' walakini hamyatendi nisemayo?" Na katika Mathayo 24:11-12, anasema, "na manabii wengi wa uongo watatokea na kudanganya wengi. Na kwa sababu ya kuongezeka maasi, upendo wa wengi utapoa." Yesu alitambua uasi wa sheria kama kipengele katika ujumbe wa walimu wa uongo. *Uasi wa sheria wa Mungu* ndio msingi wa ukristo bandia! Manabii wa uongo kwa maneno wanamkubali Yesu kama "Bwana" na kutotii sheria zake (Luka 6:46). Yesu mwenyewe alituonya katika Mathayo 7:15, "Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali." Walimu wa uasi wanaonekana kama kondoo wasio na hatia, watu wa hekima, wa ukweli wanaojisughulisha, wanaoshikilia mambo ya kidini, lakini sio wa Kristo. Watakuja kwa nguvu na uwezo, lakini tazama kipengele kikuu cha uongo, ambayo ni uasi; "Wengi wataniambia siku ile, 'Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?' Ndipo nitawaambia dhahiri, 'Sikuwajua ninyi kamwe; Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!'" (Mathayo 7:22-23).

**Sasa, Utajuaje ya Kwamba Wewe ni Mkristo?**

Ili kukuwa Mkristo, mmoja lazima awe na Roho ya Mungu. Mtume Paulo anatuambia, "Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si Wake" (Warumi 8:9). Lakini utaweza kujua kwa njia gani ikiwa unayo Roho wa Kristo? Mtume Petro anatuambia, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38). Mmoja anapaswa kutubu *dhambi* ili kuwa Mkristo. Mmoja hawezi kutubu dhambi ikiwa hajui dhambi ni nini. Baada ya kutubu mtu anapaswa kuacha kuishi katika dhambi, na ili kufanya hivyo lazima ajue dhambi ni nini. Hii inatuongoza katika swali lingine: "Dhambi ni nini?" 1 Yohana 3:4 linatuambia dhambi ni nini: "Kila atendaye dhambi, afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi." Mmoja lazima aache kuzivunja amri za Mungu ili awe Mkristo. Ikiwa mmoja anaishi maisha ya kuzivunja sheria za Mungu, basi anaendelea kuishi maisha ya dhambi na hana Roho wa Mungu. Mbona? Kwa sababu Mungu hutoa Roho wake kwa "wote wamtiio" (Matendo 5:32). Unaweza kuuliza, "kutii nini?" Ni nini tunastahili kutii ili tuweze kupokea Roho wa Mungu? Yesu alijibu swali hili wakati yule kijana tajiri alimwuliza jinsi ya kuingia katika uzima: '"Lakini ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri.' Akamwambia, 'zipi?' Yesu akasema, 'usiue,' 'usizini,' 'usiibe,' 'usishuhudie uongo,' 'waheshimu baba yako na mama yako,' na 'mpende jirani yako kama nafsi yako'" (Mathayo 19:17-19).

Unaweza kusema kwamba Yesu hakutaja Sabato ya kila wiki au ya kila mwaka kwa hivyo sizo sehemu za amri anazotutarajia kuzishika. Lakini tafakari kuihusu. Sabato sio tu amri ambayo Yesu hakuzingatia. Yesu hakutaja mengi mengine ambazo utakubali zinapaswa kutazamwa na Wakristo wote. Kwa mfano, hakutaja Amri ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu, ambazo ni: "Usiwe na miungu mingine ila mimi", "Usijifanyie sanamu ya kuchonga… usivisujudie wala kuvitumikia"; "Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako" (Kutoka 20:3-7). Je, ukweli kwamba Yesu hakutaja amri hizi tatu inamaanisha kuwa hazipaswi kushikwa? Bila shaka hapana. Sasa mbona amri ya nne ("Ikumbuke siku ya Sabato uitakase" – aya ya nane) haikutajwa? Haina maana kutoa moja na sio zingine. Ukweli ni kwamba kusudi la Yesu haikuwa kutumia Amri Kumi lakini kutumia zile ambazo yule kijana tajiri hakuwa anazitazama.

Mtume Yakobo anaiweka wazi kuwa amri zote lazima zishikwe anaposema, "Maana mtu awaye yote atakayeshika sheria yote, ila akijikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. Kwa maana yeye alisema, Usizini, pia alisema Usiue. Basi ijapokuwa hukuzini, lakini umeua, umekuwa mvunja sheria" (Yakobo 2:10-11). Hii inamaanisha wazi kuwa mmoja anayekataa kutazama Sabato za Mungu anaendelea kuvunja sheria Zake na kuishi katika hali ya dhambi.

Lakini, unaweza kusema hakuna anayezishika amri kwa ukamilifu, kwa hivyo sisi zote ni wavunja sheria. Hata wale wanaotafuta kuzishika amri za Mungu wanazivunja wakati mwingine.

Tofauti iko wapi? Tofauti ni, wale wanaokataa kushika amri za Mungu, pamoja na Sabato Zake wanafanya dhambi kimakusudi, wakati wale wanaotafuta kuzishika amri Zake hawafanyi hivyo. Mfalme Daudi anaiweka hivi: "Umzuie mtumishi wako asitende mambo ya kiburi, yasinitawale mimi. Ndipo nitakapokuwa kamili, name nitakuwa safi, sina kosa lililo kubwa" (Zaburi 19:13). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatoa ilani, "Kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi" (Waebranea 10:26).

Hatuwezi, sisi wenyewe, kuzishika sheria kwa ukamilifu. Mtu anahesabiwa haki sio kwa sheria lakini na Kristo. Biblia hata hivyo, inatuambia kwamba Kristo anawahesabia haki wale wamtiio tu. "Kwa sababu sio wale wasikiao sheria walio wenye haki mbele za Mungu, bali ni wale watendao sheria watakaohesabiwa haki" (Warumi 2:13).

**Kwa Nini Mungu Alituma Roho Wake?**

Ili kujua ikiwa tunao Roho wa Mungu, ni muhimu kuelewa kwa nini Mungu hutupatia Roho wake. Hebu turudi kwenye Agano la Kale tuchunguze. Katika Kumbukumbu la Torati, Mungu alilamikia watu wake kwa kutozishika sheria Zake. "Laiti wangekuwa na moyo kama huu ndani yao siku zote, wa kunicha, na kushika amri zangu zote siku zote, wapate kufanikiwa wao na watoto wao milele" (Kumbukumbu la Torati 5:29). Hili ndilo lilikuwa jambo lililomfanya Mungu kuona haja ya kubadilishwa kiroho itakayowawezesha watu wake kuzishika amri Zake. Mungu baadaye alitangaza kupitia nabii Ezekieli jinsi atakavyofanya hivi: "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, name nitatia roho mpya ndani yenu, name nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu [*Mbona?*] na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda" (Ezekieli 36:26-27).

Ni mpango huu wa hatua wa kutia roho wa mwanadamu kwa kuzishika amri Zake lililomfanya Mungu kuunda agano litakalojulikana kama Agano Jipya. Watu wengi wanadai kwamba wao ni Wakristo wa Agano Jipya bila ya kuelewa maana ya Agano Jipya au kwa nini ulikuwa katika uwepo. Hii imewaongoza watu wengi kuamini kwamba Agano Jipya ulikuja kuitangua sheria za Mungu, wakati kinyume chake ndicho kweli. Kusudi la Agano Jipya ni *kuwawezesha waaminio kuzishika sheria za Mungu*. Hivi ndivyo Mungu alivyotangaza Agano Jipya katika Agano la Kale:

"Angalia, siku zinakuja, asema BWANA, nitakapofanya Agano Jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda. Si kwa mfano wa agano lile nililofanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri; ambalo agano langu hilo walilivunja, ingawa nalikuwa mume kwao, asema BWANA. Bali agano hilo ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema BWANA; nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu." (Yeremia 31:31-33; tazama pia Waebrania 8:8).

Sheria haimo tena kwenye vidonge vya jiwe bali kwenye mioyo kupitia Roho. Bila ya Roho wa Mungu hatuwezi kumtii. Tunahitaji Roho wa Mungu kwa sababu “Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana Haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu” (Warumi 8:7-8).

**Hitimisho**

Kwa sababu tunaishi katika tamaduni ya kuvunja Sabato, kuipuuza Sabato haionekani kwetu kama kutenda dhambi. Kama wale wanaoishi katika jamii zinazokubalii mwanaume kuwaoa wake wengi hawatamwona kama mtendaji wa dhambi, au vile kanisa zingine hazina ugumu wa kuwachukua kuhani walio katia uhusiano wa jinsia moja kwa sababu hii inakuwa jambo la kawaida katika jamii zetu. Watu wengi hupata dini yao kutoka kwa tamaduni zao. Lakini Wakristo wa kweli hawawezi kutumia tamaduni zao kuamua jinsi Mungu anavyopaswa kuabudiwa.

Wengi huamini kwamba wanaweza kuwa Wakristo wa kweli na kuishi maisha ya kuvunja Sabato. Walakini watu hawa hawa hawatakubali kwamba wanaweza kuwa Wakristo wa kweli na kuishi maisha ya kuzini. Ni kwa msingi gani watu huhitimisha kwamba Amri ya Nne inayoshughulikia Sabato, haina umuhimu kuliko Amri ya Saba, inayoshughulikia kuzini? Ni wapi katika Biblia mmoja huweza kupata dai hili likiungwa mkono? Yesu alisema, “Basi mtu yeyote atakayevunja amri moja katika hizi zilizo ndogo, na kuwafundisha watu hivyo, ataitwa mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni; bali mtu atakayezitenda na kuzifundisha, huyo ataitwa mkubwa katika ufalme wa mbinguni” (Mathayo 5:19).

Sio ngumu baada ya yote kutofautisha kati ya Ukristo wa kweli na ule wa uongo. Uasi wa sheria ndicho alama ya Ukristo bandia. Hii ndio hoja Mtume Yohana anatuelezea katika 1 Yohana 2:3-6:

“Na katika hili, twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake. Yeye asemaye, ‘nimemjua’ wala hazishiki amri zake, ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake. Lakini yeye alishikaye neno lake, katika huyo upendo wa Mungu umekamilika kweli kweli. Katika hili twajua ya kuwa tumo ndani yake. Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda.”

Yesu alienendaje? Yesu mwenyewe anatuambia katika Yohana 15:10, “Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.” Ndio, “Ukitaka kuingia katika uzima, zishike amri” (Mathayo 19:17). Haina shaka kwamba katika sura ya mwisho ya kitabu cha mwisho ya Biblia Yesu alifunua maneno haya kwa Mtume Yohana kama aina fulani ya ukumbusho wa mwisho: “Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake” (Ufunuo 22:14-15).

Mwandishi: George Ramocan